MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA IRINGA (IRINGA WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-021-2018/2019

Mnamo tarehe 10 Januari 2019 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Iringa (Iringa WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2017/18	Madabiliko yanayopendekezwa kwa asilimia	2018/19	Madabiliko yanayopendekezwa kwa asilimia	2019/20	Madabiliko yanayopendekezwa kwa asilimia	2020/21
Majumbani							
Daraja 1 (1-5m^3)	1,685	32%	2,222	-3%	2,155	1%	2,177
Daraja 2 (6-20m^3)	1,820	57%	2,857	-3%	2,771	1%	2,799
Daraja 3 (>21m^3)	2,035	45%	2,945	-3%	2,857	1%	2,885
Taasisi							
Daraja 1 (1-5m^3)	1,645	50%	2,462	-3%	2,388	1%	2,412
Daraja 2 (6-40m^3)	1,900	50%	2,843	-3%	2,758	1%	2,786
Daraja 3 (>41m^3)	2,035	45%	2,945	-3%	2,857	1%	2,885
Biashara							
Daraja1 (1-10m^3)	1,555	50%	2,327	-3%	2,257	1%	2,280
Daraja 2 (>10m^3)	1,790	50%	2,679	-3%	2,598	1%	2,624
Viwanda							
Daraja 1 (1-10m^3)	1,760	73%	3,045	-3%	2,954	1%	2,983
Daraja 2 (>10m^3)	2,035	57%	3,200	-3%	3,104	1%	3,135
Magati	1000	30%	1,300	-3%	1,261	1%	1,274

Jedwali Na 2: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa za Huduma ya Majitaka (Shilingi/Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	Asilimia 40 ya Gharama za Maji	Asilimia 40 ya Gharama za Maji	Asilimia 40 ya Gharama za Maji	Asilimia 40 ya Gharama za Maji
Taasisi	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji
Biashara	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji
Viwanda	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji	Asilimia 80 ya Gharama za Maji

Jedwali Na 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	20,000	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 24 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2013.		
Taasisi	30,000			
Biashara	30,000			
Viwanda	50,000			
Magati	25,000			

Jedwali Na 4: Ada ya Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi/Marejesho)

Kundi la Sasa	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2017/18	Madabiliko yanayopendekezwa kwa asilimia	2018/19	Madabiliko yanayopendekezwa kwa asilimia	2019/20	Madabiliko yanayopendekezwa kwa asilimia	2020/21
Majumbani	20,000	0%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Taasisi	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Biashara	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Viwanda	45,000	0%	45,000	0%	45,000	0%	45,000
Magati	35,000	0%	35,000	0%	35,000	0%	35,000

Jedwali Na 5: Tozo ya Sasa na Zinazopendekezwa za Gari la Majitaka (Shilingi/Safari)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Inayopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani (Nje ya Mtandao wa Majitaka)	75,000	75,000	75,000	75,000
Wasio Majumbani (Nje ya Mtandao wa Majitaka)	85,000	85,000	85,000	85,000
Majumbani (Ndani ya Matandao wa Majitaka)	130,000	130,000	130,000	130,000
Wasio Majumbani (Ndani ya Matandao wa Majitaka)	140,000	140,000	140,000	140,000

Jedwali Na 6: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Zinazopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21
Majumbani	3,000	Kuondoa Tozo ya Huduma kwa Makundi Yote ya Wateja		
Taasisi	4,000			
Biashara	4,000			
Viwanda	4,000			
Magati	3,000			

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa, sababu kuu za kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni ongezeko la gharama za uendeshaji na matenengezo, uhitaji wa fedha kugharamia ukarabati, ununuzi wa vifaa na miradi, kulipa tozo zilizopo kisheria (kama vile Ushuru wa Uendelezaji Ufundi Stadi), na kufidia upungufu wa mapato unaotokana na kuondolewa kwa tozo ya huduma.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 21 Februari 2019** katika **Ukumbi wa Siasa ni Kilimo** uliopo Iringa Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi.** Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Iringa, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu **ifikapo tarehe 22 Februari 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA KATI, GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA IRINGA.**

Imetolewa na:

Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)

6 Februari 2019